

MBOLEA BORA KWA KILIMO ENDELEVU

# Mbolea YETU




Tanzania


ISSN 2799-2039

Toleo Na. 05 - Januari - Juni 2023

## Tathmini yabainisha RUZUKU YA MBOLEA Ilivyochocha wakulima kuongeza tija



Wakulima nchini  
wachekelea miaka  
miwili ya Rais  
Samia – **Uk.7**



Temu: Kilimo kimo  
kwenye damu yangu,  
nataka kumiliki  
hekta 1,000 – **Uk.10**

## UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI

### Wakulima changamkieni fursa ya ruzuku ya mbolea

**Maelfu** ya wakulima walionufaika na mpango wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa 2022/2023 wana hadithi ndefu ya kuwasimulia wenzao ambao hawakubahatika kijiungu na mpango huo.

Mpango huu wa ruzuku ya mbolea umebuniwa na serikali ili kuimarisha sekta ya kilimo na kuchochea ongezeko la pato la taifa na hatimaye kuwatuirisha wakulima ambao kwa miongo mingi walishindwa kupiga hatua za maana katika ustawi wao.

Katika Tanzania zimepita kampeni nyingi zilizolenga kuimarisha kilimo tangu kupatikana kwa uhuru zaidi ya miaka 60 iliopita. Nyingi ya kampeni hizo zilifanikiwa kuleta hamasa miongoni mwa wakulima ili waongeze tija katika uzalishaji wa mazao mbalimbali. Hata hivyo, kwa bahati mbaya kampeni hizo hazikuwa endelevu kiasi cha kuwakwamua wakulima waondokane na umaskini.

Ndiyo maana katika kukifanya kilimo chetu kiwe endelevu na kilete tija kwa wakulima serikali imebuni mpango huu wa ruzuku ya mbolea ili kuzalisha chakula kwa wingi na kupata malighafi viwandani kwa bidhaa zitokanazo na juhudzi za wakulima wanaounda uti wa mgongo wa uchumi wa taifa.

Ni jambo la kutia moyo kwamba baada ya kubaini mafanikio yatokanayo na mpango huu wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa 2022/2023 serikali kwa kauli moja imeamua kuuendeleza kwa misimu mingine "kuanzia 2023/2024 hadi 2025/2026." Sasa hivi kinachosuburiwa ni maelekezo ya serikali jinsi mpango huu utakavyotekelozwa kwa misimu hiyo miili.

Nia ya serikali ni kuwawezesha mamilioni ya wakulima wazidi kunufaika na ruzuku ya mbolea ili kuchochea kukua kwa uchumi wa taifa. Vyama vya ushirika vilivyozagaa nchi nzima ni lazima vijipange kikamilifu katika utekelezaji wa mpango huu huko vijijini.

Nijukumula serikali za mitaa huko vijijini zisaidie usimamizi wa bei elekezi ya mbolea kwa kila kituo kutegemeana na mazingira halisi ya sehemu inayohusika. Tunatarajia kwamba vituo vya mauzo ya mbolea vikiwa karibu na wakulima, kundi hilo la wachapa kazi wa Tanzania litahamasika zaidi katika kutumia mbolea ili kukuza uzalishaji.

Kampeni hii ya ruzuku ya mbolea ni lazima iote mizizi katika ngazi zote kuanzia vitongoji, vijiji, kata na tarafa – maeneo ambayo kuna idadi kubwa ya wananchi. Viongozi wa ngazi zote kuanzia vijiji hadi taifa ni lazima wasimame kidete kuhakikisha kampeni hii inafanikiwa kwa sababu imebuniwa kumkomboa mkulima wa Tanzania katika karne hii inayoshuhudia maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia.

Miaka ya mwanzo ya uhuru, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, altuasa kutimiza wajibu wetu ili kujiletea maendeleo. Kwa sasa hamasa hii ni lazima ihamie kwa wakulima kwa kuwataka wajisajili kwa wingi ili waweze kufaidi matunda ya ruzuku ya mbolea. Kwa njia hiyo watakuwa wanapiga vita umaskini na kubadili hali zao za maisha.

Ni vizuri kwa Watanzania kuchangamkia fursa kama hizi zinazotolewa na serikali ambazo zinalenga kubadili maisha yao baada ya miongo mingi ya kuelewa kwenye dimbwi la umaskini.



Dkt. Stephan Eliuth Ngailo  
Mukurugenzi Mtendaji

### BODI YA UHARIRI

**DKT. STEPHAN NGAILO**  
- MWENYEKITI

**MATILDA KASANGA**  
- KATIBU

**DANIEL MAARIFA**  
- MJUMBE

**RAYMOND KONGA**  
- MJUMBE

**AZIZI MTAMBO**  
- MJUMBE

**SALEHE KEJO**  
- MJUMBE

**THERESIA SIRIWA**  
- MJUMBE

**NURU MWASAMPETA**  
- MJUMBE

**ALPHA NUHU**  
- MJUMBE

# TAHARIRI

## Ukombozi kwa vijana utaletwa na kilimo

KWA vijana wengi walioonja matunda ya kilimo, ni vigumu leo hii kuwarudisha nyuma kwa kuwashawishi waiache kazi hiyo na kuanza kukimbia mijini kutafuta kazi kama ilivyokuwa zaidi ya miongo mitatu iliyopita.

Miaka ya 1980 na 1990 ilishuhudia wimbi kubwa la vijana wa Tanzania wakihama vijihi vyao na kukimbia mijini wakidhani kwamba huko ndiko kwenye maziwa na asali. Hali hiyo ilivinyang'anya vijihi vingi nguvukazi muhimu katika kuendeleza, siyo tu kilimo, bali pia sekta nyingine za kiuchumi.

Ni jambo la kusikitisha kwamba shughuli za kilimo ziliachwa mikononi mwa wazee na hivyo kusababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao muhimu ya biashara na chakula. Maisha ya vijijini yalionekana kana kwamba ni laana; vijana walikimbilia kujazana mijini ambako huko walidhani kila kitu utakikuta mezani bila kuvuja jasho. Hiyo ilikuwa ni dhana potofu na itaendelea kuwa potofu hadi milele.

Leo hii mambo yamebadilika; ari ya maelfu kwa maelfu ya vijana kukimbia mijini imefifia kwa sababu hata mijini wanakokimbilia maisha ni machungu kwa kuwa hakuna kazi za maana za kuwasaidia kujenga ustawi wao.

Vijana wengi sasa – ambao wengi wao wamepata mwanga wa elimu -- wameelewa kwamba maisha ni kujituma na siyo kuyakimbia kama ilivyokuwa miaka kadhaa huko nyuma. Maisha, kama walivyowahi kusema wanafalsafa wengi, ni mapambano ; kwamba popote ulipo ni lazima uparibane ili uweze kufanikiwa. Uelewa huu ndiyo uliowafanya vijana wengi sasa kujikita katika kilimo – kiwe cha mazao ya chakula au biashara.

Sasa hivi tunashuhudia vijana wakianzisha mashamba ya mpunga kama ilivyo Wami Dakawa, Madibira, Shinyanga na kwingineko kunakolimwa zao hilo kwa wingi. Sasa hivi tunawashuhudia vijana wanaomiliki mashamba ya parachichi katika mikoa kama vile Mbeya, Njombe na Iringa. Huu ni ukombozi wa kifikra.

Huu pia ni uthibitisho kwamba kilimo sasa kinalipa kwa mtu ye yote aliyeamua kujitosa katika sekta hiyo inayoajiri mamilioni ya Watanzania. Zama za vijana kuchagua kazi ya kufanya zimepitwa na wakati. Hizo zilikuwa ni zama ambazo wasomi walikuwa na kiburi na majivuno kwa kuchagua aina ya kazi kwa sababu wataalam enzi hizo walikuwa wachache kuziba uhaba uliokuwepo.

Leo hii litakuwa ni jambo la kustaaajabisha ikiwa vijana wa Tanzania wataendelea kuinung'unikia serikali kwamba haiwapi kazi za kufanya. Katika nchi yenye ardhi ya kutosha na yenye rutuba tunatarajia kwamba nguvukazi ya vijana itatumika vilivyo kuwakombua na tatizo la ukosefu wa ajira.

Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuwakombua vijana kwa kuwasaidia wajajiri kwenye kilimo. Ni juu ya vijana wenye sasa kuitumia fursa hii kwa makini ili waweze kuondokana na dhana iliyodumu kwa miaka mingi ya kupapatikia ajira za serikali.

Vijana wa leo wanatakiwa kuiga maneno ya Mtengenezaji Filamu wa Marekani, Walt Disney, aliyetamka kwamba "Ndoto zetu zinaweza kuwa za kweli iwapo tutakuwa na ujasiri wa kuzifikia." Kujikita katika kilimo kutawasaidia vijana wanaoota ndoto za mafanikio kuweza kuufikia utajiri.

# U K O M B O Z I T A Y



Serikali yaamua mbolea ya ruzuku iendelee kutolewa hadi 2026

**Uk > 5**



Wakulima 3,149,824 wajisajili mfumo wa ruzuku ya mbolea

**Uk > 6**



Bashe ataja vipaumbele, mikakati ya kukuza kilimo 2023/2024

**Uk > 12**



Mbolea ya ruzuku: Fursa lukuki kwa wafanyabiashara

**Uk > 13**

Orodha ya Mbolea na Visaidizi vya Mbolea zilizosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009

**Uk > 15**



Wahariri wa Vyombo mbalimbali vya Habari wakitembelea kiwanda cha mbolea cha itracom mara baada ya kikao cha siku mbili na viongozi waandamizi wa Wizara ya Kilimo na watendaji wake iliyowajengea uwezo katika shughuli mbalimbali zinazotekelzeza na wizara na taasisi zilizo chini ya wizara

## Tathmini yabainisha ruzuku ya mbolea Ilivyochochea wakulima kuongeza tija

### • Waomba mpango huo uendelee

Na MWANDISHI WETU

**MPANGO** kabambe wa kitaifa wa ruzuku ya mbolea uliobuniwa na serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan kuimarisha sekta ya kilimo iweze kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa taifa umechochea hamasa kubwa mionganoni mwa wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali, kwa mujibu wa tathmini iliyofanya na Mamlaka ya Udhhibitii Mbolea Tanzania (TFRA) kuhusu utekelezaji wa mpango huo.

Tathmini ya TFRA imeonyesha kuwepo mwitikio mkubwa kutoka kwa wakulima baa da ya kupunguza makali ya bei ya mbolea ili waweze kuongeza tija katika kilimo.

Hapo Julai 4, 2023 serikali ilizindua rasmi Mfumo wa Kidijitali wa Usajili wa Wakulima na kutoa Mwongozo wa Utoaji wa Mbolea ya Ruzuk kwa msimu wa kilimo 2022/2023 baa da ya kutenga shilingi billioni 150 ili zitumike kuboresha mpango huo.

Lengo kubwa la ruzuku ya mbolea kwa ujumla wake ni kupunguza bei ya bidhaa hiyo ili kuwahamisisha wakulima waongeze uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula nchini na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

TFRA ni taasisi ya serikali ilioanzishwa zaidi ya miaka 10 iliyopita na kukabidhiwa jukumu la kudhibiti ubora wa mbolea inayozalishwa ndani na kuingizwa kutoka nje. Taasisi

hiyo, ambayo imepata mafanikio makubwa katika muongo uliopita, pia iilipewa jukumu la kuhakikisha kwamba mikakati ya usambazaji mbolea ya ruzuku inafanikiwa kuboresha sekta ya kilimo nchini.

Akitoa tathmini ya utekelezaji wa mpango huo wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 katika mahojiano maalum, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo aliorodhesha mafanikio kadhaa, yakiwemo kuwatumbau wakulima na wadau wote walioko kwenye mnyororo wa thamani wa mbolea, na kujua takwimu halisi za mahitaji ya pembejeo hiyo kwa nchi nzima.

Alisema kumekuwepo na mwamko mkubwa mionganoni mwa wakulima wa kununua mbolea na hiyo kuchochaea ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao mbalimbali licha ya changamoto ya hali mbaya ya hewa iliyojitokeza katika baadhi ya maeneo nchini.

"Tunategemea uzalishaji mkubwa wa mazao mbalimbali katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambako kulikuwa na mvua za kutosha," ameeleza Dk. Ngailo, na kuongeza kuwa "tumegundua kwamba bei ya mbolea ikiwa nafuu, mwamko wa wakulima wa kununua bidhaa hiyo unakuwa ni mkubwa zaidi."

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, hadi kufikia Mei 3 mwaka huu jumla ya wakulima 3,050,419 walikuwa tayari wamesajiliwa nchini kupata mbolea ya ruzuku.

Kuhusu changamoto mbalimbali zilizoji-

tokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo, Dk. Ngailo alisema kulikuwepo na ukosefu wa uaminifu mionganoni mwa mawakala, hasa kuhusu uhaliisa wa taarifa za mauzo na ununuzi wa mbolea.

Changamoto nyingine kubwa ni ukosefu wa mtaji kwa mawakala huko vijiji. Kati ya mawakala 350,000 waliosajiliwa ni mawakala 1,200 tu ndio waliokuwa na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika programu ya ruzuku wakati wengine walobaki wakiwa hawana fedha za kutosha kushiriki katika zoezi hilo.

"Hali hii," alieleza Dk. Ngailo, "iliathiri usambazaji wa mbolea licha ya kuwepo hamasa kubwa mionganoni mwa wakulima, wafanya-bashara, mawakala na wadau wote."

Jambo la kufurahisha na kutia moyo, Dk. Ngailo alisema, ni kwamba wadau wote kwenye mnyororo wa thamani wa mbolea wameishukuru serikali kwa kuanzisha mpango huo wa ruzuku na kuitaka ijithadi kuboresha mfumo mzima wa upatikanaji wa pembejeo hiyo ili kuongeza tija katika sekta muhimu ya kilimo. TFRA imekuwa ikipigana kufa na kupo na ili kufanikisha ongezeko la viwanda nya mbolea na visaidizi vyake nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Katika uhamasishaji wa uzalishaji wa mbolea nchini, TFRA imefanikisha kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea nchini kwa asilimia 41, matumizi ya mbolea kwa ongezeko la asilimia 31 na ongezeko la mbolea zilizosajiliwa kwa asilimia 45.

Mafanikio hayo, kwa mujibu wa Dk. Ngailo, ni jitihada za makusudi za kututua changamoto mbalimbali kwenye tasnia ya mbolea na kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

Pamoja na mafanikio hayo machache katika mengi ambayo hayajaainishwa, TFRA ina matarajio makubwa, ikiwemo kumalizika kwa maabarwa ya mbolea, kuimarishwa ofisi za kanda, kuongeza idadi ya waguzi wa mbolea nchini, kuongeza utii wa sheria kwa asilimia 90, kuongezeka kwa viwanda nya uzalishaji wa mbolea na kuwa na mfumo wa uhakika wa upatikanaji wa takwimu.

# Serikali yaamua mbolea ya ruzuku iendelee kutolewa hadi 2026



**Na MWANDISHI WETU**

**Serikali** imeamua kuendelea kuratibu utoaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima hadi mwaka 2025/2026 ili kuchocha hamasa ya matumizi ya pembejeo hiyo kutoka kilo 19 kwa hekta hadi kufikia kilo 50 kwa hekta.

Waziri wa Kilimo Hussein Bashe aliliambia

*Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe,  
akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Bajeti  
ya wizara kwa mwaka 2023/2024 Jijini  
Dodoma, Mei 8 mwaka huu.*

Bunge wakati akiwasilisha Makadirio ya Bajeti ya wizara yake kwa mwaka 2023/2024 jijiini Dodoma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) inaendelea na usajili wa wakulima katika mfumo wa kidigitali ili kufifanya taifa liwe na takwimu na taarifa sahihi.

Alisema serikali kuitia TFRA itaendelea kuratibu uingizwaji wa tani 750,000 za mbolea nchini na kwamba Wizara ya Kilimo itaiwezesha Kampuni ya Mbolea (TFC) kupata shilingi bilioni 40/- kama mtaji na hivyo kuongeza mtaji huo kufikia shilingi bilioni 46 kwa ajili ya kununua mbolea na ardhi ya kujenga kivanda cha kuchanganya mbolea kwa kushirikiana na sekta binafsi.

"Hاتua hii inalenga kupunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje na kuimarisha upatikanaji wake kulingana na afya ya udongo ya eneo husika," alisema.

Akizungumzia upatikanaji wa mbolea, Bashe alisema wizara kuitia TFRA ilipanga kuratibu uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa tani 650,000 za mbolea kwa msimu wa 2022/2023 ulioishia Juni mwaka huu.

Hadi kufikia Aprili mwaka huu upatikanaji wa mbolea ulifikia tani 819,442 ikiwa ni asilimia 126 ya lengo.

Kiasi hicho kimetokana na tani 75,399 zilizozalishwa nchini, tani 617,079 zilizoagizwa kutoka nje na tani 126,964 ikiwa ni bakaa ya msimu wa 2021/2022, alisema Bashe, na kuongeza kuwa hili ni ongezeko la asilimia 46 ikilinganishwa na msimu wa 2021/2022 ambapo upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 560,553.



*Waziri wa Kilimo Hussein Bashe (mwenye kofia SSH) akizungumza na Meneja wa Kampuni ya ETG kanda za Nyanda za Juu Kusini Trusher Darji alipotembelea ghalia la kampuni hiyo eneo la vivanda Iyunga mkoani Mbeya Januari mwaka huu.*

# Wakulima 3,149,824 wajisajili mfumo wa ruzuku ya mbolea



Bwana Shamba wa Kampuni ya ETG mkoani Arusha Isdory Kayanda akieleza namna wakulima walivonyufaika na mbolea ya ruzuku alipotembelewa na timu ya wataalamu wa mawasiliano wa Mamlaka ya Udhhibit wa Mbolea Tanzania.

Na MWANDISHI WETU

**Wakulima** wapata 3,149,824 nchini wamesajiliwa katika mfumo wa kidigitali ambapo kati yao 826, 336 wamenufaika na mpango wa ruzuku ya mbolea kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Akiwasilisha Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024 Waziri wa Kilmimo Hussein Bashe alisema kwa mara ya kwanza katika historia ya

Tanzania, serikali imewatambua wakulima walionufaika na mbolea ya ruzuku kwa majina yao kamili, mahali walipo, aina ya mazao na ukubwa wa mashamba na maeneo yao wanayofanya shughuli za kilimo.

Aidha waziri alisema serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibit wa Mbolea Tanzania itaendelea na zoezi la kusajili wakulima na kutoa kadi lengo ikiwa ni kuwasajili wakulima 7,000, ooo ifikapo 2025.

"Zoezi hili litaunganisha kanzidata na satelite, taarifa za afya ya udongo kwa kila mkulima na huduma za ugani ili Taifa liweze kuwa na uhakika wa takwimu za wakulima", alisema Waziri Bashe.

Amesema waingizaji wakubwa wa mbolea 28, mawakala wadogo, 3, 265 na wazalishaji wa ndani watatu wamesajiliwa katika mfumo wa ruzuku ya mbolea ili kuhakikisha kuwa usambazaji wa mbolea unafanikiwa.



Mkulima wa mpunga na mnufaika wa mbolea ya ruzuku katika Mkoa wa Kilimanjaro akipalilia shamba lake.



Mkulima wa viazi, Hermengildi Temu, wilayani Siha akikagua shamba lake lililoathiriwa na ukame. Mkulima huyo aliishkuru serikali kwa kutoa ruzuku ya mbolea iliyomwezesha kkupuanu shamba lake.



Mwonekano wa jengo la maabara ya kimataifa ya mbolea Eneo la Kilimo III Temeke, Jijini Dar es Salaam. Maabara hiyo inatarajiwa kuwa kitovu cha huduma na taarifa mbalimbali kuhusu tasnia ya mbolea kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

# Wakulima nchini wachekelea miaka miwili ya Rais Samia

Na MWANDISHI WETU

**"Kwa** mwaka jana nilipaswa kutumia kiasi cha shilingi 18,000,000 kwa ajili ya mbolea ili kulima hekta 20 za nanasi. Nilifanikiwa kulima kulima hekta mbili tu kwa sababu ya bei kubwa ya mbolea. Sasa nimeweza kununua mifuko 30 ya mbolea ya kuanzia ninapoendelea kuandaan maeneo mengine kwa ajili ya kilimo."

Hayo ni maneno ya Mubaraka Mtenga, mkulima wa nanasi wa kijiji cha Fukayo-si wilayani Bagamoyo akielezea furaha yake baada ya serikali kutoa ruzuku ya mbolea na hivyo kuwawezesha wakulima kupanua mashamba yao ikilinganishwa na misimu mingine iliyopita.

Naye Mkulima wa vitunguu, mahindi, maharage na mbogamboga wa eneo la Mang'ola



wilayani Karatu, Mustapha Mbwambo, anasema amepata nafuu sana ya uzalishaji wa vitunguu baada ya serikali kuanza kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima katika msimu wa kilimo 2022/23.

Anasema msimu wa 2021/2022 gharama ya mbolea ilikuwa kubwa na hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji kutokana na hekta moja ya vitunguu kuhitaji mifuko 12 ya mbolea. Anaelea kwamba ruzuku ya mbolea imewapunguzia mzigo wakulima na kuwawezesha kuongeza maeneo ya kilimo.

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua mpango wa ruzuku ya mbolea Agosti 8 mwaka jana wakati wa maadhimisho ya Siku Wakulima iliyofanyika viwanja vya Mwangan-gale jijini Mbeya.

## Sababu ya serikalikuanzisha mpango wa mbolea ya ruzuku

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhidhi Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo anasema kwamba kupanda kwa bei ya mbolea kwenye soko la dunia kumesababisha wakulima wengi kutoweza kumudu gharama za bidhaa hiyo na kui lazimisha Serikali ya Awamu ya Sita kutenga shilingi bilioni 150 ili kughamaria ruzuku kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023.

>>> **Inaendelea Uk. 8**



### <<< Inatoka Uk. 7

Mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 gharama za mbolea zilipanda kwa ghafla na wakulima walinunua bidhaa hiyo kwa bei ya kuanzia shilingi 100,000 hadi 150,000 kufutana na umbali wa kupatikana kwa bidhaa hiyo.

Kwa mujibu wa Dkt. Ngailo utoaji wa ruzuku ya mbolea umezingatia mahitaji halisi ya mkulima wa Tanzania kulingana na taarifa za usajili na bajeti ya serikali. Mbolea zilizohusika katika mpango wa ruzuku ni zile za kupandia na kukuzia, hasa DAP na Urea. Mbolea hizo ni takribani asilimia 50 ya matumizi yote ya mbolea nchini.

Mbolea za kupandia na kukuzia za aina nyiningine zimehusishwa kwenye ruzuku kulingana na mahitaji ya soko. Mbolea zinazozalishwa na viwanda vya ndani zimeingizwa kwenye mpango wa ruzuku kutokana na mahitaji ya soko.

Katika kuhakikisha malengo ya kutoa ruzuku yanafikiwa, ikiwa ni pamoja na kuwanufaisha wakulima,, kuongeza ufanisi wa utoaji wa ruzuku, kupunguza mianya ya udanganyifu, rushwa, muda na gharama za usimamizi kutokana na uzoefu uliopatika-

*Jengo la utawala la kiwanda cha mbolea cha Itracom Jijini Dodoma. Kiwanda kinatarajiwa kumaliza changamoto ya upatikanaji wa mbolea na kupunguza utegemezi kwa mbolea kutoka nje.*

na wakati wa utekelezaji wa mipango ya ruzuku kwa miaka iliyopita, serikali iliama kutumia mfumo wa kidijitali kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mfumo umetumia programu maalum ya kidigitali, au kwa Kiingereza Digital Platform, kuratibu shughuli zote za utekelezaji ruzuku kuanzia utambuzi wa washiriki wa mfumo wakiwemo waingizaji na wazalishaji wa mbolea, wafanyabiashara, wakulima na aina za mbolea zitakazokuwa katika mpango wa ruzuku; kuratibu usambazaji; uuzaaji wa mbolea kwa wakulima; na malipo ya ruzuku ya mbolea.

Dkt. Ngailo anabainisha kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2023 waingizaji wa mbolea 28 walikuwa wameshasajiliwa, wazalishaji 3, mawakala na wasambazaji wa mbolea 3,303 watakaotumika kusambaza mbolea katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

### Kuongezeka kwa viwanda vya kuten-geneza mbolea na visaidizi vya mbolea (fertilizer suppliments)

Akizungumzia kuhusu ongezeko la viwanda vya mbolea na visaidizi vyake, Dkt. Ngailo anaeleza kuwa kutokana na utashi wa kisiasa na uhamasishaji uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kumekuwa na jumla ya viwanda kumi na saba (17) vinyoyozalisha aina mbalimbali za mbolea na visaidizi vyake.

Kati ya viwanda 16 viwanda 3 huzalisha visaidizi vya mbolea (chokaa mazao na gypsum) vilivyoko mikoa ya Dodoma na Tanga viwanda 14 vinatengeneza mbolea za punje na maji ambapo kati ya hivyo 10 hutengeneza mbolea za maji na 6 hutengeneza mbolea za punje.

Aidha, Rais Dkt. Samia na serikali yake wameendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza ambapo mwekezaji kutoka nchini Burundi yupo katika hatua za mwisho za ujenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer LTD kinachojengwa Nala Jijini Dodoma ambacho tayari kimeanza uzalishaji wa tani 200,000 kwa mwaka na baada ya mitambo yote, kiwanda kitazalisha tani 1,000,000 za mbolea na tani 300,000 za chokaa na hivyo kusaidia

**Kutokana** na utashi wa kisiasa na uhamasishaji uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kumekuwa na jumla ya viwanda kumi na saba (17) vinavyozalisha aina mbalimbali za mbolea na visaidizi vyake.



**Mifumo** ya udhibiti wa mbolea nchini imeendelea kuimashwa na kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea bora kwa bei nafuu na kwa wakati ndani ya miaka miwili ya Rais, Dkt. Samia

kupunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi.

#### **Ujenzi wa maabara kupima mbolea**

Dkt. Ngailo anaeleza kuwa Mamlaka imetuwa ikitumia maabara za taasisi nyininge kupima ubora wa mbolea ambapo kumekuwa na ucheleweshaji wa kutoa majibu na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya udhibiti.

Anasema ndani ya iongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mamlaka ilitengewa ba-jeti na kuanza kutekeleza ujenzi wa maabara ya mbolea kwa njia ya force account ambapo hadi mwezi Februari 2023 ujenzi wake ulifikia asilia 95.

Maabara ya mbolea inatarajiwu kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na kutumiwa na nchi jirani za Malawi, Zambia, Jamhuri ya KLidemokasi ya Congo, Burundi na Rwanda na hivyo kuongeza mapato ya nchi.

#### **Hali ya upatikanaji wa mbolea**

Akielezea kuhusu hali ya upatikanaji wa mbolea nchini chini ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Dkt. Samia, Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Joseph Charos anasema kwa mwaka 2020/2021 hali ya upatikanaji wa mbolea ilikuwa ni tani 546,818 ambapo matumizi yalikuwa tani 475,870 na mpaka kufikia Januari, 2023 hali ya upatikanaji wa mbolea nchini imefikia tani 678,528, sawa na asilimia 102 ya mahitaji ya mbolea ambapo matumizi yalikadiriwa kuwa tani 667,730 mwishoni mwa mwezi Juni mwaka huu.

#### **Hali ya Udhibiti wa Mbolea nchini**

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Happiness Mbele, anasema mifumo ya udhibiti wa mbolea nchini imeendelea kuimashwa na kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea bora kwa bei nafuu na kwa wakti. Anasema udhibiti umewezekana kufuatia kuongezeka kwa idadi ya wakaguzi wa mbolea, kusajili wafanyabiashara, na kutoa mafunzo ya mara kwa mara juu ya mfumo wa uendeshaji wa biashara ya mbolea.

Kuanzia mwaka 2012 mpaka sasa kuna wakaguzi wa mbolea 140 kutoka katika Ofisi za Mamlaka na Halmashauri za Wilaya, Aidha maafisa kilimo 59 kati ya 140 walipata mafunzo ya ukaguzi na wanasubiri kutangazwa kwenye gazeti la serikali ili waendelee na jukumu la Kudhibiti ubora wa mbolea.

#### **Kuongezeka kwa idadi ya wafanya-biashara wa mbolea**

Mafanikio mengine ndani ya tasnia ya mbolea chini ya uongozi wa Rais. Dkt. Samia ni kuongezeka kwa wafanyabiashara wa mbolea nchini. Kufuatia uwepo wa mazingira rafiki ya

biashara, idadi ya wafanyabiashara wa mbolea imeongezeka kutoka 1,691 mwaka 2020/2021 hadi kufikia wafanyabiashara 4,776 mwezi Februari mwaka huu.

“Hayo ni mafanikio makubwa kwani yanangeza nguvu ya usambazaji wa bidhaa hiyo kwa wakulima,” anaeleza Mbele.

#### **Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea**

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka tani 426,550.41 mwaka 2021/ 2022 hadi tani 667,730 kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limetokana na utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea ulioamsha ari ya wakulima kuongeza maeneo yao ya kilimo na elimu ya matumizi sahihi ya mbolea inayotolewa na Mamlaka kwa wakulima ili kuwawezesha kuongeza tija kwenye kilimo chao.

#### **Kufunguliwa kwa ofisi za kanda**

Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Victoria Elangwa, anaeleza kuwa miaka miwili iliyopita Mamlaka ilikuwa na ofisi moja tu ambayo ndiyo ilikuwa makao makuu ya Mamlaka Jijini Dar es Salaam. Hali hiyo iliwafanya wadau kutumia muda mrefu kupata huduma ambazo zingewachukua muda mfupi kuzipata endapo wangekuwa na ofisi katika maeneo jirani wanakofanyia shughuli zao.


Anasema ndani ya miaka miwili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Mamlaka ilifanikiwa kufungua ofisi tano za Kanda -- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Kati (Tabora), Kanda ya Kaskazini (Arusha), na Kanda ya Ziwa (Mwanza).

#### **Kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma**

Kwa upande wake, Meneja wa Kitengo cha Tehama, Robert Mtendamema anaeleza kuwa katika kipindi cha miaka miwili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Mamlaka imefanikiwa kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma kwa wadau wake ambapo huduma zote zinatolewa kuititia Mfumo wa Kimtandao wa Mbolea (FIS).

Anasema kuwa mfumo huo unahudumia wadau ikiwa ni pamoa na wanaohitaji kujisajili kufanya biashara ya mbolea, kusajili mbolea mpya, waingizaji wapya wa mbolea na wale wanaowasilisha maombi ya vibali vya kutoa na kuingiza mbolea nchini ambapo awali huduma zote zilikuwa zikitolewa kwa mfumo wa analogia na hivyo kutumia muda mrefu na kuhusisha kusafiri ili kukamilisha mahitaji ya wadau.

Mafanikio haya yanahitimisha Agenda 10/30: Kilimo ni Biashara ikibeba maana ya kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la taifa na kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 kuwa halisi kufuatia tija inayopatikana kuititia uimarishaji wa tasnia ya mbolea nchini.



# Temu: Kilimo kimo kwenye damu yangu, nataka kumiliki hekta 1,000

Na MWANDISHI WETU

**"Wakati** baba yangu ananipeleka shule ya seminari ya Mtakatifu James mkoani Kilimanjaro miaka ya 1970, nilikuwa na uhakika sitahudumu kama mtumishi wa Mungu katika maisha yangu."

"Nilimwambia kwa uwazi baba yangu kuhusu suala hilo na kwamba ndoto yangu ilikuwa kushirikiana naye katika shughuli za kilimo.

Haya ni maneno ya Hermengildi Temu au Karume, kama anavyofahamika huko wilayani Sija, mkoani Kilimanjaro.

Temu aliyasema hayo katika mazungumzo na waaandishi wa habari walipotembelea shamba lake walipofanya ziara katika Kanda ya Kaskazini. Waandishi hao wa habari walifanya ziara ya kutathmini mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa serikali kuwapatia wakulima mbolea ya ruzuku katika msimu wa kilimo wa 2022/23.

"Hivyo ndivyo ushiriki wangu katika kilimo ulivoanza. Niliungana na baba yangu moja kwa moja katika shughuli za kilimo baada ya kuhitimu masomo yangu," anasema.

"Kuanzia hapo, kilimo kimekuwa sehemu ya maisha yangu na eneo langu la kitaalamu," anaongeza Temu, ambaye pamoja na kilimo cha viazi mbatata amejikita pia katika kilimo cha ngano na maharagwe.

Anasema analima viazi mbatata katika eneo lenye ukubwa wa ekari 400, ekari 250 zaidi ya eneo alilokuwa analima msimu uliopita kabla serikali haijaanzisha utoaji wa mbolea kwa ruzuku.

Kwa mujibu wa Temu, uamuza wa kuongeza ekari 250 unatokana na nafuu aliopata kufuatia utolewaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima hivyo kumpunguzia yeze na wakulima wengine gharama za uendeshaji.

Hata hivyo, anasema kwa ari aliyonayo hivi sasa anatamani kufanya shughuli za kilimo katika eneo kubwa zaidi ikibidi serikali imsaidie kupata ekari 1,000 za ardhi.

"Nimekuwa nikiendesha shughuli zangu katika ardhi ya kukodi na kuniongezea gharama za uendeshaji. Serikali ifikirie namna inavyoweza kusapoti wananchi wake walionyesha nia na utayari wa kuwekeza katika kuleta mageuzi ya kilimo kwa kuwapatia ardhi ya kutosha," anasema.

"Hatua hiyo si tu itaongeza mavuno, bali itachangia kwa kiasi kikubwa katika ongezeko la mapato yatokanayo na kilimo yanayokusanywa na halmashauri," anaongeza.

Anasema amekuwa akichangia wastani wa Shilingi Milioni Nane hadi Milioni 12 kwa mwaka katika mapato yanayokusanywa na halmashauri ya wilaya ya Sija.

Kwa mujibu wa Temu, wakulima watakoongeza eneo la kilimo wataongeza mavuno, hivyo kuvuna mazao zaidi na kujihakikishia ongezeko la kipato wao binafsi na

**Nimekuwa** nikiendesha shughuli zangu katika ardhi ya kukodi na kuniongezea gharama za uendeshaji. Serikali ifikirie namna inavyoweza kusapoti wananchi wake walioonyesha nia na utayari wa kuwekeza katika kuleta mageuzi ya kilimo kwa kuwapatia ardhi ya kutosha

**Lori** moja ni sawa na wastani wa gunia 150 hadi 160 za viazi mbatata. Wakati gunia moja huuzwa kwa wastani wa Shilingi 80,000 sokoni, mkulima hupata Shilingi 60,000 hadi Shilingi 70,000 anapouza shambani

halmashauri zao.

#### Kilimo cha viazi mbatata

Temu anasema ili kufanikiwa katika kilimo cha viazi mbatata, ameajiri mameneja wanane wanaomsaidia katika shamba lake.

"Mameneja hawa si wahitimmo wa elimu ya juu, bali ni watu wenye uzoefu wa kutosha niliofanyanao kazi kwa muda mrefu kama vibarua," anasema.

"Ni watu walioonyesha uwezo mkubwa wa kusimamia wenza na wanauelewa mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusiana na kilimo," anaongeza.

Kwa mujibu wa Temu, uelewa wake kuhusu kilimo bora ni mkubwa kutokana na kufanyakazi katika sekta hiyo kwa muda mrefu.

Anasema amekuwa akipitisha uzoefu huo kwa mameneja wake ili utekelezaji ufanwyne na wafanyakazi wanaoajiriwa shambani mwake.

"Kwa kawaada nimekuwa nikikubaliana na mameneja hawa kuwalipa kiasi kidogo cha fedha na kiasi kikubwa hulipwa wakati wa mavuno. Mara nyingi malipo hulingana

na thamani ya kipato cha mavuno ya eka mbili hadi tatu," anasema.

Anasema kwa wastani, eka moja ya shamba la viazi mbatata hutoa gunia 15 hadi 20 ya mavuno endapo mbolea hajatumika.

"Wastani wa gunia 70 hadi 100 hupatikanwa toka kwenye shamba ambalo mbolea imetumika," anasema Temu.

Anasema kwa kawaada viazi mbatata kuto ka kwenye shamba lililotumia mbolea vina soko zaidi kwa vile ni vikubwa ikilinganishwa na viliviyunwa toka kwenye shamba ambalo mbolea hajatumika.

#### Uwekezaji

Temu anasema anatumia wastani wa Shilingi Milioni 100 hadi Milioni 150 kwa msimu katika shughuli zake za kilimo, huku akiwatahadharisha wawekezaji katika sekta hiyo kuwa na subra.

Anasema kilimo ni sawa na mtoto mchanga anayejifundisha kutembea hivyo wawekezaji na wananchi wanatakiwa kuvumilia changamoto zote zitakazojitekeza.

"Wanapaswa kuwa wavumilivu kwa sababu watapitia vipindi vigumu vyenye kuvunja moyo vikiambatana na mavuno hafifilicha ya kufanya uwekezaji mkubwa," anasema.

"Wanaweza kupata mavuno makubwa msimu wa kwanza, lakini mkulima atapaswa kujianaa changamoto zinazoweza kujitokeza kwa misimu mitatu hadi minne mfululizo," anaongeza.

Kwa mujibu wa Temu, wakulima wanapaswa kutunza rasilimali kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza.

Hata hivyo, aliyahakikishia watananza kuwa kilimo hakina presha kama ilivyo kwenye sekta zingine.

#### Mbolea ya ruzuku

Temu anapongeza uamuzi wa serikali kuwapatia wakulima mbolea ya ruzuku, akitijolea mfano kuwa anatumia nusu ya fedha alizokuwa anatumia awali kwa ajili ya ununu wa mbolea.

Anasema ametumia jumla ya mifuko 700 hadi 1,400 aliyoidhinishwa kwa ajili ya kilimo msimu huu.

"Wakulima hawapaswi kukata tamaa kwani wanapofikia hatua hiyo ndipo wenza wanapoandikisha mafanikio. Ni dhambi kubwa kukata tamaa kwenye kilimo," anabainisha.

Licha ya kuishukuru serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwapatia wakulima mbolea ya ruzuku, alitoa rai akitaka ifikirie kujumisha dawa za kuua wadudu katika orodha ya pembejeo za kilimo zinatolewa kwa mfumo wa ruzuku.

"Licha ya kuhitajika kwa wingi, dawa hizo zinapatikana kwa bei ya juu sana halii inayofanya wakulima wengi washindwe kumudu," anasema Temu.

"Pia maofisa kilimo wanapaswa kutembelea wakulima katika maeneo yao na kuwapa ushauri wa kitaalamu utakaoboresha na kuleta mapinduzi ya kilimo nchini," anasema.

Kwa mujibu wa Temu, msimu huu kilimo kimeathiriwa na changamoto ya mabadi-liko ya tabianchi, hivyo kuiomba serikali kuwapatia wakulima kiasi kingine cha mbolea ya ruzuku katika msimu mpya unaoanza mwezi Machi 2023.

"Hii ni kwa sababu wakulima wengi wanametumia sehemu kubwa ya mbolea walioyidhinishwa katika msimu wa kilimo ambao umeathiriwa na ukame," anasema.

#### Soko la viazi mbatata

Temu anasema baadhi ya wafanya-biashara hufuata viazi mbatata shambani na kwamba wakati mwininge wakulima hulazimika kusafirisha bidhaa hiyo hadi soko la Mabibo jijini Dar es Salaam.

Vinapofikishwa jijini Dar es Salaam, bidhaa hiyo huwekwa chini ya usimamizi wa madalali ambao huingiza fedha za mauzo katika akaunti za benki za wakulima.

Anabainisha kuwa lori 60 za viazi mbatata ndicho kiasi kikubwa cha mavuno alichowahi kupata tangu alipoanza kujihusisha na kilimo cha zao hilo.

"Lori moja ni sawa na wastani wa gunia 150 hadi 160 za viazi mbatata. Wakati gunia moja huuzwa kwa wastani wa Shilingi 80,000 sokoni, mkulima hupata Shilingi 60,000 hadi Shilingi 70,000 anapouza shambani," anasema.

#### Changamoto

Changamoto kubwa, kwa mujibu wa Temu, ni kuwa viazi mbatata vinahitaji mvua nydingi na kiwango kikubwa cha dawa za kuua wadudu.

"Tatizo ni kuwa dawa hizo huuzwa kwa bei kubwa na kwamba hazijajumuishwa kwenye mpango wa ruzuku wa serikali," anabainisha.

#### Manufaa

Anasema kilimo cha viazi mviringo kimemuwezesha kutunza familia vizuri na kuwapatia elimu bora watoto wake.

Temu anasema mtoto wake wa kwanza ni mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), huku wengine wawili wameolewa na mmoja amejikita kilimo kama yeye.

"Nimemshauri mtoto wangu mkubwa aangalau uwezekano wa kujingiza kwenye kilimo licha ya kuajiriwa katika utumishi wa umma," anasema Temu mwenye umri wa miaka 60.

Pia anasema amewekeza katika biashara ya vituo ya mafuta hasa katika makazi yake ya kudumu eneo la Tarakea, wilayani Rombo, Kilimanjaro.



Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zake wakifuatilia uwasilishaji wa bajeti ya wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## Bashe ataja vipaumbele, mikakati ya kukuza kilimo 2023/2024

Na MWANDISHI WETU

**Wizara** ya Kilimo imesema katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeazimia kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula kwa kujilisha yenye wena pia kwa kunufaika kwa kuyalisha mataifa mengine kibashara na hivyo kuimarisha ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alilimbia Bunge wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Bajeti ya wizara hiyo kwamba kwa mwaka wa fedha 2023/2024 lengo ni kuifanya sekta ya kilimo kuwa endelevu itakayowapa fursa vijana na wanawake kushiriki kwenye kilimo biashara.

"Lengo ni kutoa fursa za ajira zenye staha na kipato cha uhakika ili kufikia lengo la ukuaji wa sekta ya kilimo na kuondoa watu kwenye umaskini," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2023/2024 serikali imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vitakavyotekelawa kupitia mikakati 26. Kipaumbele namba moja kitakuwa kuongeza tija katika uzalishaji, hasa uwekezaji kwenye maeneo ya kimakatia kama vile utafiti wa mbegu bora, uzalishaji wa mbegu na miche bora, usambazaji wa mbegu na miche ya ruzuku na uwekezaji kwenye huduma za ugani.

Kipaumbele kingine ni kuongeza ajira zenye



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akielekea Bungeni kuwasilisha Makadirio ya Bajeti ya wizara yake kwa mwaka 2023/2024.

staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza upatikanaji wa ardi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoa.

Pia kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kupitia programu ya Jenga Kesho iliyo Bora na kuendeleza vituo mahiri vya kusambaza teknolojia, alisema waziri huyo.

Alisema kipaumbele kungine ni kuimarisha usalama wa chakula na lishe ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimakatia kama vile miundombinu ya uhifadhi kufikia uwezo wa kuhifadhi tani milioni tatu ifikapo 2023.

Alitaja kipaumbele kingine ni kuimarisha upatikanaji wa masoko mitaji na mazao ya mazao nje ya nchi. Alisema kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimakatia kwa kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika Halmashauri.

Bashe alitaja maeneo mengine ni kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi na kuiwezesha sekta binafsi kwa kujengeta miundombinu ya masoko na kuongeza mazao ya mazao nje.

Kipaumbele kingine ni kuimarisha upatikanaji wa masoko mitaji na mazao nje ya nchi na kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimakatia yakiwemo ya kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika Halmashauri mbalimbali.

Kipaumbele cha tano ni kuimarisha maendeleo ya ushirika kwa kuboresha usimamizi na udhibiti wa vyama vya ushirika, kuwezesha vyama vya ushirika, kuijidesha kibashara na kuvisaidia kupata mitaji na kuimarisha na kupitia upya mifumo ya upatikanaji wa viongozi wa vyama vya ushirika.

Bashe alisema mpango na Bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umelenga kujenga sekta ya kilimo endelevu itakayowapa fursa vijana na wanawake kushiriki kwenye kilimo biashara.

Alisema maeneo ya uwekezaji ni ujenzi wa miundombinu ya umwagiiaji, miundombinu ya uhifadhi, uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoa, upatikanaji wa pembejio, utafiti na huduma za ugani.

Bashe aliwaeleza wabunge kuwa Bajeti ya Wizara ya Kilimo imendelea kuongeza kwa mafungu yote matatu na katika mwaka 2023/2024, bajeti imongezeka kutoka sh. 751,123,280,000 hadi sh. 970,785,619,000, sawa na ongezeko la asilimia 29.24.

Alisema fedha hizo zimetengwa kuimarisha utafiti wa kilimo, uzalishaji wa mbegu, utoaji wa ruzuku kilimo cha umwagiiaji, miundombinu ya uhifadhi wa mazao, kuimarisha huduma za ugani, upatikanaji wa masoko ya mazao na kuendeleza programu ya Jengo Kesho iliyo Bora.

